Kivunge cha Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi



Kivunge cha Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi



Dibaji

Wanafunzi wamekuwa wakiandaliwa kushiriki katika shughuli za kidemokrasia wakiwa shuleni kupitia somo la Uraia. Pamoja na kuwa na somo hili katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari ushiriki wa wanafunzi katika masuala ya kidemokrasia hauridhishi. Utafiti uliofanywa na HakiElimu mwaka 2022 kwa ufadhili wa Mfuko wa Demokrasia wa Umoja wa Mataifa (UNDEF) katika wilaya sita (6) za Tanzania Bara ambazo ni Mkuranga, Tabora, Ukerewe, Kilwa, Sumbawanga, na Arusha, na kuhusisha shule 24 za umma na binafsi umeonesha kuwa wanafunzi wengi hasa wenye umri wa kuanzia miaka 14 hadi 19 hawashiriki kikamilifu katika shughuli za kidemokrasia.

Matokeo ya utafiti yalionesha somo la Uraia lina mada zinazolenga kuwajengea wanafunzi umahiri wa demokrasia. Hata hivyo, kuna vikwazo kadhaa katika utekelezaji wa muhtasari wa somo la Uraia. Vikwazo hivyo ni pamoja demokrasia kuhusishwa zaidi na suala la uchaguzi wa viongozi shuleni, uhaba wa walimu mahiri, somo kupangiwa muda mfupi wa kufundishia na kujifunzia, pamoja na kukosekana kwa sheria na sera jumuishi zinazohusu ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za kidemokrasia nje ya mfumo wa shule.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti, HakiElimu imebaini umuhimu wa kukuza umahiri wa demokrasia kwa wanafunzi, uzalendo na uwajibikaji. Kivunge hiki kinalenga kulea na kukuza ushiriki wenye maana wa wanafunzi kwenye mfumo na maisha ya kidemokrasia kuanzia darasani, nje ya darasa na kwenye jamii wanamoishi. Pia kinalenga kuwawezesha wanafunzi kuwa wazalendo wenye kuwajibika katika shughuli zao za kila siku. Aidha kinatoa njia, mbinu na mikakati ya kuwawezesha walimu na wanafunzi kuwa chachu ya kuwajibika kidemokrasia na kuwa raia wema. Vile vile kinatoa fursa kwa wazazi na jamii kuwa sehemu ya mchakato wa kuleta na kuthamini ushiriki wenye manufaa wa wanafunzi katika maeneo yote ya maisha.

Kwa kubuni na kuandaa kivunge hiki kinachotokana na ushahidi wa kisayansi, HakiElimu inachangia katika jitihada za serikali na wataalamu wa elimu kutafuta utatuzi wa changamoto zilizopo katika elimu. Ni matumaini yetu kuwa matokeo ya utekelezaji wa kivunge hiki katika shule za majaribio utatoa matokeo yatakayowezesha Taifa letu kuwaandaa wanafunzi na kuwafungulia fursa za kushiriki katika masuala ya kidemokrasia ndani na nje ya shule.

Dkt. John Kalage
Mkurugenzi Mtendaji
HakiElimu

Shukrani

Maandalizi ya kivunge hiki yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka ndani na nje ya Shirika. HakiElimu inatoa shukrani za dhati kwa Pius Makomelelo, Naomi Mwakilembe, Irene Kanyankole, Boniventura Godfrey, Dkt. Wilberforce Meena, Gaudence Kapinga, Dkt. Perpetua Kalimasi na Peter Bandio kwa kuandaa kivunge hiki. Aidha, pia inawashukuru Elisante Kitulo, na Dkt. John Kalage kwa kuhariri.

Muundo na Matumizi ya Kivunge

Kivunge hiki kimeandaliwa katika mfumo wa moduli ambazo maudhui yake yametokana na matokeo ya utafiti uliofanywa na HakiElimu kwa lengo la kubaini jinsi somo la Uraia linavyowaandaa wanafunzi kushiriki katika michakato mbalimbali ya kidemokrasia na kutambua haki na wajibu wao kama raia. Kivunge hiki kina moduli kuu mbili ambazo zina vipengele sita. Moduli ya kwanza inahusu ukuzaji wa demokrasia, uzalendo na uwajibikaji kwa wanafunzi shuleni. Moduli hii inalenga kuzifanya shule kuwa sehemu muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kujenga maana pana ya demokrasia zaidi ya kuihusisha na siasa pamoja na uchaguzi. Moduli ya pili imejikita katika kuwawezesha wanafunzi kuhawilisha umahiri wa demokrasia na misingi ya uzalendo wanayoyajenga shuleni kwenye maisha yao ya kila siku katika jamii.

Kwa ujumla, moduli zinalenga kuimarisha mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia na kujenga ari ya uzalendo kwa kumwezesha mwanafunzi kujadili na kushiriki katika kupanga na kutoa uamuzi kuhusu mambo yanayoendelea katika ngazi ya darasa, shule na jamii kwa ujumla. Aidha, uwezeshaji kupitia moduli hizi unamuweka mwanafunzi kuwa mlengwa mkuu katika kujifunza, kumjengea stadi za uongozi kama mchochea mabadiliko ndani na nje ya shule huku akitambua haki na wajibu wake kwa Taifa. Kila moduli ina kazi kuu, kazi mahususi na tafakuri.

Watumiaji wakuu wa kivunge hiki ni walimu wawezeshaji ambao wanafundisha somo la Uraia kidato cha kwanza mpaka cha tatu katika shule ishirini za sekondari za majaribio. Shule hizi zipo katika wilaya za Mkuranga, Kilwa, Sumbawanga, Ukerewe, Arusha na Manispaa ya Tabora. Walimu hawa watatafsiri kwa vitendo walichojifunza katika kivunge hiki katika ufundishaji wao ndani ya darasa na katika shughuli za ziada za mtaala. Pia watawawezesha walimu wengine kukielewa kivunge na kukitumia katika kazi zao kwa kuzingatia ratiba ya shule. Katika ngazi ya jamii utekelezaji wa kivunge hiki utawezeshwa na wawezeshaji jamii kwa ushirikiano wa karibu na shule. Lakini pia kivunge hiki kinaweza kutumiwa na wadau wengine wa elimu wenye shabaha ya kuwawezesha wanafunzi kushiriki kikamilifu na kuwajibika katika michakato ya kidemokrasia na kujenga ari ya uzalendo.

Utekelezaji wa kivunge hiki utafuata hatua kuu zifuatazo:

01

Kuandaa shule na jamii kuelewa na kukubali kutoa nafasi zaidi kwa wanafunzi kukuza uwezo wao katika masuala ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji.

02

Shule kuwaandaa walimu na wafanyakazi wengine kutekeleza kivunge hiki kwa kuingiza maudhui yake kwenye mpango wa shule.





03

Shule kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kivunge.

Yaliyomo

Dibaji ii

Shukrani iii

Muundo na Matumizi ya Kivunge iv

Moduli 1: Maeneo, Mbinu na Mikakati ya Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi Shuleni

1.1. Ujifunzaji na Ufundishaji 3

Kazi kuu 4

1.1.1. Kuimarisha uelewa wa walimu kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia 4

1.1.2. Kuimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia 5

Tafakuri 6

1.2. Uongozi na Utawala wa Shule 7

Kazi kuu 8

1.2.1. Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kushirikisha wanafunzi kwenye uamuzi 8

1.2.2. Kuimarisha mifumo ya wanafunzi kupaza sauti 9

Tafakuri 11

1.3. Uongozi wa Wanafunzi 12

Kazi kuu 13

1.3.1. Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kuthamini demokrasia katika uongozi wa wanafunzi 13

1.3.2. Kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika uongozi wao na uzalendo 14

1.3.3. Kuimarisha uchaguzi wa viongozi wa wanafunzi 15

Tafakuri 16

1.4. Kuimarisha Shughuli za Ziada za Mtaala katika Kukuza Umahiri wa Demokrasia 17

Kazi kuu 18

1.4.1. Kuimarisha umahiri wa demokrasia na uzalendo kwenye klabu za masomo 18

1.4.2. Kuimarisha na kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika michezo kwa kuzingatia mahitaji yao 19

1.4.3. Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali 21

1.4.4. Kukuza na kuendeleza maadili ya kidemokrasia na ari ya uzalendo 23

Tafakuri 24

Moduli 2: Mbinu na Mikakati ya Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi kwenye Jamii 27

Kazi Kuu 29

2.1. Kuandaa Utayari wa Jamii 29

Tafakuri 30

Kazi Kuu 31

2.2. Kuimarisha Ushiriki wa Wanafunzi kwenye Shughuli za Kijamii 31

Tafakuri 32

Kiambatisho: Mwongozo wa tathmini 33

Viashiria vya utendaji na vigezo vya tathmini 33



Moduli 1:

Maeneo, Mbinu na Mikakati ya Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi

Shule ni taasisi yenye jukumu kubwa katika kuwaandaa wanafunzi kuishi katika jamii ya kidemokrasia, kuwa raia wema na wawajibikaji. Ili kufikia shabaha hii shule inatakiwa kutoa mwanya kwa wanafunzi kushiriki vya kutosha katika shughuli mbalimbali za shule ambazo zitawajengea maarifa, stadi na mwelekeo utakaowawezesha kuwa washiriki hai katika jamii yenye mila, desturi na utamaduni tofauti. Demokrasia, uzalendo, na uwajibikaji ni dhana mtambuka ambazo zinajitokeza kwenye ujifunzaji na ufundishaji, utawala, uongozi na shughuli za ziada za mtaala.

Malengo ya moduli hii ni:

01 Kuimarisha maarifa, stadi na mwelekeo wa walimu na wanafunzi kuhusu demokrasia, uzalendo na uwajibikaji.

02 Kuwezesha walimu kufundisha kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na kuhusisha nadharia na vitendo.

03 Kuimarisha uongozi na utawala wa kidemokrasia kwenye shule.

04 Kuwezesha mazingira ya kujifunza kuwa ya kidemokrasia.

1.1. Ujifunzaji na Ufundishaji

Mwanafunzi ndiye mlengwa mkuu kwenye ujifunzaji na ufundishaji hivyo katika mazingira ya kujifunza ya kidemokrasia huwajibika zaidi katika ujifunzaji wake. Katika shule nyingi nchini, mwanafunzi amekuwa mpokeaji zaidi wa maarifa kutoka kwa mwalimu. Mtazamo wa kisasa unamchukulia mwalimu kama mwezeshaji ambaye jukumu lake ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza kwa kutumia njia, mbinu na mikakati ambayo inamfanya kuwa kitovu cha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Msisitizo upo katika kumwezesha mwanafunzi kujenga tabia ya kujifunza katika maisha yake yote.

Malengo:

- Kuimarisha maarifa, stadi na mwelekeo wa walimu kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia.
- Kuimarisha matumizi ya mbinu na mikakati ya demokrasia katika ujifunzaji na ufundishaji.

Kazi Kuu

1.1.1. Kuimarisha uelewa wa walimu kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia

Ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia utafanikiwa kama walimu watauelewa kwa kina na kuutekeleza. Ili kufanikisha lengo hili, walimu wote wanatakiwa kupewa fursa ya kukuza umahiri wao kwenye dhana ya demokrasia na jinsi ya kufanya mchakato wa kujifunza kuwa wa kidemokrasia. Shule nyingi zimeweka mkazo katika kukamilisha mihtasari ya masomo na kujifunza kwa ajili ya kufanya mitihani zaidi badala ya kuwajengea wanafunzi umahiri. Katika hali hii walimu kwa pamoja wanapaswa kuwa waumini wa kweli wa demokrasia na kuizingatia kwenye utendaji wao. Ni muhimu kutambua kwamba wanafunzi wengine wanaweza kuwa na utendaji wa juu kama demokrasia itatamalaki kwenye mchakato wa kujifunza na kufundisha. Kazi mahususi zifuatazo zitawezesha walimu kuboresha maarifa, stadi na mwelekeo wao kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia.

Kazi Mahususi

1.1.1. Mwalimu Mwezeshaji kuandaa mafunzo ya walimu wote kujadili na kukubaliana kuhusu dhana ya ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia demokrasia kwa kufanya yafuatayo:

- Kutoa taarifa ya mafunzo wiki moja kabla kwa walimu baada ya kuwasiliana na uongozi wa shule.
- Kuainisha malengo ya mafunzo na kuwatumia walimu wote kabla ya siku ya mafunzo. Malengo hayo ni:
    - Kujadili njia, mbinu na mikakati ya ufundishaji ambayo mwanafunzi anakuwa kitovu cha ujifunzaji.
    - Kujadili mahusiano ya kidemokrasia kati ya mwanafunzi na mwalimu wakati wa kujifunza.
    - Walimu wajadili faida na changamoto za kufundisha kidemokrasia na jinsi ya kuzikabili.
    - Kujadili mikakati na rasilimali ya utekelezaji unaozingatia muktadha wao.

Kazi Kuu

1.1.2. Kuimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia

Wanafunzi ni walengwa wakuu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji shuleni. Mchakato wowote wa kufanya walimu kufundisha kwa kuzingatia misingi ya demokrasia utakuwa na matokeo chanya kama walimu na wanafunzi wataukubali na kuutumia. Baadhi ya wanafunzi hawafurahii matumizi ya njia, mbinu na mikakati ambayo inawafanya wao kuwa washiriki wakuu kwenye mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Wakati mwingine wanafunzi wanapenda walimu wanaokuwa chanzo cha maarifa bila ya kutambua umuhimu wa wao kuwa na nafasi kubwa kwenye mchakato wa kufundisha na kujifunza.

Kazi Mahususi

1.1.2.1 Mwalimu Mwezeshaji aandae kikao cha muda usiozidi saa moja kuwaelimisha wanafunzi kuhusu ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia demokrasia kwa kufanya yafuatayo:

- Kutoa taarifa ya uwepo wa kikao kwa wanafunzi wote kupitia madarasa na mbao za matangazo.
- Kuainisha malengo ya kikao husika ambayo ni pamoja na:
    - Kujadili mahusiano ya kidemokrasia kati ya mwanafunzi na mwalimu wakati wa ujifunzaji.
    - Kujadili mahusiano ya kidemokrasia baina ya wanafunzi katika kujifunza.
    - Kujadili mbinu za ufundishaji wa kidemokrasia.
    - Kuainisha faida na changamoto katika mchakato wa Ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia ukuzaji wa demokrasia na jinsi ya kuzitatua.
- Mwalimu Mwezeshaji ashirikiane na wanafunzi kuandaa maelezo kwenye karatasi ngumu yanayobainisha manufaa ya ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia demokrasia kisha wazibandike kwenye mbao za matangazo.



Tafakuri

Mwalimu Mwezeshaji ataongoza tafakuri mara moja kila mwezi ambapo wanafunzi na walimu watatoa maoni yao kwa maandishi na kisha kuyajadili kwenye vikao. Sambamba na maoni ya wanafunzi, pia Mwalimu Mwezeshaji atashirikiana na mwalimu wa taaluma kupata mrejesho kutoka kwa viongozi wa madarasa kuhusu ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia kanuni za kidemokrasia. Katika hili Mwalimu Mwezeshaji kwa kushirikiana na mwalimu wa taaluma watabainisha mambo makuu yaliyojitokeza kwenye maelezo ya wanafunzi, viongozi wa madarasa na mwalimu na kupanga tarehe ya kuyapitia. Kutakuwa na vikao viwili, kikao cha kwanza kitakuwa cha Mwalimu Mwezeshaji na walimu wenzake na kikao cha pili kitakuwa cha Mwalimu Mwezeshaji na wanafunzi. Katika kikao cha wanafunzi walimu wengine wanaweza kuhudhuria ili kutanua wigo wa majadiliano. Maelezo ya walimu na wanafunzi yatahifadhiwa kwenye mkoba wa kazi wa Mwalimu Mwezeshaji. Maswali yafuatayo yatatumika ambapo swali moja au mawili yanaweza kujibiwa katika kikao kimoja:

- Tumepata mafanikio gani wakati wa kutumia mbinu za kufundisha na kujifunza za demokrasia?
- Mapokeo ya walimu na wanafunzi yakoje kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa demokrasia?
- Je, wanafunzi wamejenga umahiri upi wa demokrasia?
- Tumebaini faida, na changamoto zipi wakati wa kutumia mbinu za kufundishia za demokrasia?
- Tumechukua hatua gani kukabiliana na changamoto zilizojitokeza? Tumetoa suluhisho gani?



1.2. Uongozi na Utawala wa Shule

Uongozi una jukumu la kujenga utamaduni wa kidemokrasia katika shule ikiwemo kuwashirikisha wanafunzi kwa kiwango kikubwa katika ngazi ya uamuzi. Hata hivyo, tafiti mbalimbali zinaonesha shule nyingi hazitoi fursa kwa wanafunzi kushiriki kikamilifu katika uongozi wa shule. Viongozi wa wanafunzi wamekuwa wapokeaji na watekelezaji wa maagizo kutoka kwenye utawala.

Malengo:

- Kuimarisha uongozi na utawala wa shule kwa kuwashirikisha wanafunzi katika ngazi mbalimbali za uamuzi.
- Kuimarisha uwezo wa wanafunzi katika kutoa maoni yao.

Kazi Kuu:

1.2.1. Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kushirikisha wanafunzi kwenye uamuzi

Ushirikishaji wa wanafunzi katika kufanya uamuzi ni jambo la msingi sana katika kuimarisha demokrasia ndani ya shule. Uzoefu unaonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya shule, viongozi wamekuwa wakifanya uamuzi wenye athari kwa wanafunzi bila ya kuwashirikisha. Matokeo yake mapokeo yamekuwa hafifu na wakati mwingine kuleta migogoro isiyo ya msingi. Aidha, imekuwa ikidumaza uwezo wa wanafunzi kushiriki katika michakato mbalimbali ya kidemokrasia ndani na nje ya shule.

Kazi Mahususi

1.2.1.1. Mkuu wa shule aandae kikao cha uongozi wa shule kujadili mikakati ya kuwashirikisha wanafunzi kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi:

- Mkuu wa shule aitishe kikao cha walimu kuweka mkakati wa kuwashirikisha wanafunzi katika uamuzi.
- Uongozi wa shule ubainishe ngazi mbalimbali za uamuzi na namna wanavyoweza kuwashirikisha.

1.2.1.2. Uongozi wa shule kuandaa mdahalo wa pamoja kati ya viongozi na wanafunzi ili kupata maoni ya namna bora ya ushirikishaji kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi:

- Mwalimu mkuu awatangazie wanafunzi na walimu siku ya mdahalo na kuandaa ajenda.
- Uongozi wa shule na wanafunzi wakae kikao kuandaa utaratibu na kanuni za kuwashirikisha kwenye ngazi mbalimbali zenye uamuzi.
- Uongozi wa shule uweke taarifa za uamuzi, na taarifa za shule kwenye mbao za matangazo zinazoweza kufikiwa kwa urahisi na wanafunzi wengi.

Kazi Kuu:

1.2.2. Kuimarisha mifumo ya wanafunzi kupaza sauti

Ili kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika michakato ya kidemokrasia shuleni, ni muhimu kujenga mifumo sahihi itakayowezesha wanafunzi kuwa na utamaduni wa kupaza sauti zao bila woga kuanzia ngazi ya msingi (darasani). Shule nyingi kwa kuzingatia sheria ya Elimu ya mwaka 1978 zimeweka mifumo mbalimbali ya kumwezesha mwanafunzi kupaza sauti ikiwemo mikutano ya darasa, baraza la wanafunzi na mingine mingi. Lakini kiuhalisia, mifumo mingi haifanyi kazi hivyo kuwanyima wanafunzi fursa hii. Mifumo hii inapaswa kuwawezesha wanafunzi kutoa sauti zao na pia kupokea mrejesho kutoka kwa viongozi. Ili kuwezesha hili, juhudi zinahitajika kumjengea mwalimu stadi za kumwezesha mwanafunzi kutambua uwepo wake na namna bora ya kuitumia mifumo kuwasilisha hoja kupitia vikao, mikutano ya darasani, na nje ya darasa. Pia, kutoa fursa kwa wanafunzi kutumia maandishi kama sehemu ya kupaza sauti zao kupitia mbao za matangazo, sanduku la maoni, au kwa kutumia sanaa za maonyesho mfano nyimbo, ngojera, risala, na maigizo. Hii itawajengea wanafunzi kujiamini na kuwa na uthubutu wa kuelezea hisia, mitazamo na matatizo yao bila uoga.

Kazi Mahususi

1.2.2.1. Kuwajengea walimu uwezo wa jinsi ya kupokea na kutoa mrejesho wa maoni ya wanafunzi. Yafuatayo yafanyike:

- Uongozi wa Shule kwa kushirikiana na Mwalimu Mwezeshaji kuandaa mafunzo kwa walimu kuhusu namna bora ya kupokea maoni ya wanafunzi na kutoa mrejesho wenye tija. Mafunzo hayo yaguse mambo yafuatayo: fursa zilizopo zinazoweza kuchagiza wanafunzi kupaza sauti (mfano: sanduku la maoni, mbao za matangazo, sanaa za maonesho na kadhalika).
- Kuandaa mikutano au mijadala ya pamoja kati ya walimu na wanafunzi itakayowezesha kupaza sauti za wanafunzi na pia kupata mrejesho.
- Uongozi wa shule kwa kushirikiana na Mwalimu Mwezeshaji kuandaa kikao kwa wanafunzi kuhusu namna bora ya kutoa maoni. Kikao hicho kiguse njia mbalimbali za utoaji maoni na namna bora ya kutoa maoni.

1.2.2.2. Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuelewa umuhimu wa kutoa maoni, faida zake na jinsi ya kuwasilisha maoni yao. Mwalimu Mwezeshaji afanye yafuatayo:

- Kuandaa mafunzo kwa wanafunzi kuwaelewesha umuhimu wa kutoa maoni na faida zake katika mchakato wa kuimarisha demokrasia.
- Kuwaongoza wanafunzi kutengeneza misingi na kanuni za ushiriki katika mikutano na kuweka ratiba ya mikutano na mijadala itakayokubalika na uongozi wa shule.
- Kuwaongoza wanafunzi kubaini majukwaa ya kutumia kupaza sauti zao na kuweka misingi ya matumizi bora ya majukwaa hayo.

1.2.2.3. Wanafunzi kujadili changamoto zinazowakabili kupitia vikao vya madarasa, mabaraza ya shule na kuandaa utaratibu wa kuziwasilisha kwenye uongozi wa shule. Mwalimu Mwezeshaji afanye yafuatayo:

- Kuwawezesha wanafunzi kuandaa ratiba za mikutano ngazi ya darasa na shule (rejea miongozo ya shule).
- Kuandaa semina kwa viongozi wa wanafunzi juu ya namna bora ya kuwezesha mikutano na mijadala yenye mwelekeo wa kidemokrasia.
- Kuwakumbusha wanafunzi juu ya matumizi bora ya fursa za kuuliza na kujibu maswali darasani kama sehemu ya kukuza demokrasia.

1.2.2.4. Shule zianzishe masanduku ya maoni kwa ajili ya wanafunzi kupaza sauti zao. Mwalimu Mwezeshaji afanye yafuatayo:

- Kuandaa mkutano na wanafunzi kutengeneza kanuni bora na namna ya kuratibu matumizi ya sanduku la maoni.
- Kupitia kikao cha wanafunzi mwalimu mwezeshaji afafanue umuhimu wa sanduku la maoni kama nyenzo mahususi kwa wanafunzi kutoa maoni au kupaza sauti zao.
- Kuongea na uongozi wa shule kwa ajili ya manunuzi na uwekaji wa sanduku la maoni.
- Sanduku liwekwe mahali salama patakapomwezesha kila mwanafunzi kulitumia bila ya hofu (wanafunzi wapewe nafasi ya kupendekeza eneo hilo).

1.2.2.5. Kuunda kamati ya kushughulikia maoni ya wanafunzi yatokanayo na vikao vya wanafunzi na sanduku la maoni, na kutoa mrejesho wa utekelezaji. Mwalimu Mwezeshaji afanye yafuatayo:

- Kuandaa kikao na wanafunzi kwa ajili ya kutengeneza kamati ya kushughulikia maoni yao.
- Kutengeneza hadidu za rejea zitakazosaidia kuongoza utendaji wa kamati hii mfano nani atawajibika kufungua sanduku, mara ngapi kwa wiki au mwezi nk.
- Kukubaliana namna maoni yatakavyochakatwa ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu, na namna ya kutoa mrejesho kwa wanafunzi.
- Kukubaliana aina ya maoni ya kushughulikia papo kwa papo, na yale yanayohitaji kupelekwa ngazi za juu za uongozi wa shule.
- Uongozi wa shule kupitia vikao vya wazazi uhamasishe wazazi kuwaruhusu watoto wao kushiriki katika shughuli za uongozi wa wanafunzi.

Tafakuri



Mwalimu Mwezeshaji ataongoza tafakuri mara moja kila mwezi ambapo wanafunzi na walimu watatoa maoni yao kwa maandishi na baadaye kuyajadili kwenye vikao. Katika hili Mwalimu Mwezeshaji kwa kushirikiana na walimu wengine watabainisha mambo makuu yaliyojitokeza kwenye maelezo ya wanafunzi na mwalimu na kisha ataandaa vikao viwili. Kikao cha kwanza kitakuwa cha Mwalimu Mwezeshaji na walimu wenzake na kikao cha pili kitakuwa cha Mwalimu Mwezeshaji na wanafunzi. Katika kikao cha wanafunzi walimu wengine wanaweza kuhudhuria ili kutanua wigo wa majadiliano. Maelezo ya walimu na wanafunzi yatahifadhiwa kwenye mkoba wa kazi wa Mwalimu Mwezeshaji Maswali yafuatayo yatatumika ambapo swali moja au mawili yanaweza kujibiwa katika kikao kimoja:

- Je, ni kwa kiwango gani uongozi wa shule umebainisha fursa za kushirikisha wanafunzi kwenye uongozi wa shule?
- Je, ni kwa kiwango gani wanafunzi wanatumia fursa zilizopo kutoa michango yao katika uendeshaji wa shule?
- Je, mwitikio wa walimu kuhusu ushiriki wa wanafunzi kwenye uongozi wa shule ukoje?
- Je, uongozi wa shule una mfumo thabiti na fanisi wa kutoa mrejesho kwa wanafunzi?
- Je, ni kwa kiwango gani njia mbalimbali zinatumika kutoa maoni ya dharura?
- Je, wanafunzi/viongozi wana ujasiri wa kutoa maoni kwa wakati?



1.3. Uongozi wa Wanafunzi

Uongozi wa wanafunzi una nafasi kubwa katika uendeshaji na usimamizi wa maendeleo ya shule. Upatikanaji wa viongozi wa wanafunzi unapaswa kuwa wa kidemokrasia kwa kuwawezesha wanafunzi wote kushiriki kuchagua na kuchaguliwa kwa kuzingatia dhana ya uwazi, uhuru na haki. Wanafunzi wengi hawalipi uzito swala la uongozi shuleni na hivyo husababisha kukosa haki zao za kuchagua na kuchaguliwa kuwa viongozi. Wakati mwingine upatikanaji wa viongozi haufanyiki kidemokrasia, hivyo ni muhimu kwa uongozi wa shule kuwawezesha wanafunzi kuwa na uongozi imara unaopatikana kwa kushirikisha wanafunzi wote.

Malengo:

- Kuimarisha thamani ya uongozi wa kidemokrasia wa wanafunzi.
- Kuimarisha utamaduni wa kupata viongozi wa wanafunzi kwa njia ya kidemokrasia.
- Kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za uongozi shuleni.

1.3.1. Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kuthamini demokrasia katika uongozi wa wanafunzi

Ili uongozi wa wanafunzi uweze kufanya kazi zake vizuri na kwa uhuru kwa manufaa yao na shule, ni muhimu uongozi wa shule na walimu kwa ujumla waunge mkono uongozi wa wanafunzi. Hivyo, kuna haja ya kuwajengea uwezo katika masuala ya uongozi na demokrasia. Hata hivyo, viongozi wengi wa wanafunzi wanapewa majukumu bila kuandaliwa. Kwa kiasi kikubwa shule hazijaweza kuwa na utaratibu mzuri wa kuwashirikisha viongozi wa wanafunzi katika uendeshaji wa shule.

Kazi Mahususi

1.3.1.1. Uongozi wa shule kujadili umuhimu wa uongozi wa wanafunzi unaozingatia misingi ya kidemokrasia:

- Uongozi wa shule kuitisha kikao na walimu kujadili nia ya shule kuboresha demokrasia, uzalendo na uwajibikaji katika uongozi wa wanafunzi.
- Walimu na wanafunzi kutengeneza kanuni za namna walimu wanavyoweza kufanya kazi na uongozi wa wanafunzi kwa ufanisi.

1.3.2. Kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika uongozi wao na uzalendo

Wanafunzi wanapaswa kutambua umuhimu wa wao kuwa viongozi na kushiriki katika upatikanaji wa uongozi. Wanafunzi wanaposhiriki katika uongozi wa shule wanajenga tabia ya kuthamini demokrasia. Hata hivyo, wanafunzi wengi hawafuatilii kwa kina masuala ya uongozi wao ikiwemo mchakato wa upatikanaji. Hali hii imefanya baadhi ya viongozi kupatikana bila kufuata misingi ya kidemokrasia ikiwemo kuteuliwa na walimu.

Kazi Mahususi

1.3.2.1. Mwalimu Mwezeshaji kwa kushirikiana na uongozi wa shule kuandaa kikao elekezi kikilenga kukuza uelewa wa wanafunzi kuhusu uongozi bora, na umuhimu wa kushiriki kwenye chaguzi mbalimbali.

- Mwalimu atoe taarifa ya siku ya kikao elekezi na mahali itakapofanyika.
- Wawezeshaji wa kikao elekezi wawe wageni waalikwa ambao wana uzoefu wa uongozi wa wanafunzi.

1.3.2.2. Mwalimu Mwezeshaji kwa kushirikiana na wanafunzi kuunda kikundi cha wanafunzi 20 wa kike na kiume kwa ajili ya kufanya igizo kuelimisha wenzao umuhimu wa kushiriki kwenye uongozi wa shule.

- Mwalimu atoe tangazo kwa wanafunzi ili wanaopenda wawe wajumbe wa kikundi cha kuandaa igizo dhima.
- Mwalimu na wanafunzi wakubaliane muda wa kufanya mazoezi na siku igizo litakapofanyika.

1.3.2.3. Mwalimu Mwezeshaji kuandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa wanafunzi kuhusu uongozi unaozingatia misingi ya demokrasia na umuhimu wake.

- Mwalimu Mwezeshaji kupanga na viongozi siku ya mafunzo .
- Mafunzo yafanyike kwa kutumia mbinu shirikishi-Mwezeshaji anaweza kuwa mgeni mwalikwa.
- Uongozi wa wanafunzi kutengeneza ratiba ya vikao vya kujadili jinsi ya kuboresha utendaji wao na kutoa mrejesho kwa uongozi wa shule na wanafunzi.

1.3.3. Kuimarisha uchaguzi wa viongozi wa wanafunzi

Mchakato wa kuwapata viongozi wa wanafunzi unapaswa kufuata misingi ya kidemokrasia. Hata hivyo, katika baadhi ya shule, michakato ya kuwapata viongozi hutawaliwa na walimu. Hali hii inaweza kuwa kikwazo kwa wanafunzi kushiriki katika uchaguzi wa viongozi wao. Wanafunzi wakishiriki katika kupata viongozi wao, huongeza uwajibikaji na kuwajengea tabia za kushiriki katika chaguzi.

Kazi Mahususi

1.3.3.1. Kuandaa misingi ya uchaguzi wa kidemokrasia na uwajibikaji:

Ili uchaguzi uweze kufanyika kwa mafanikio kanuni ni muhimu:

- Uongozi wa shule kwa kushirikiana na wawakilishi wa wanafunzi kutengeneza kanuni za uchaguzi wa uongozi wa wanafunzi, sifa za viongozi na kuzijadili kwenye baraza la shule.
- Uongozi wa shule kushirikiana na wanafunzi kutoa andiko la kanuni za uchaguzi wa wanafunzi na sifa za viongozi na kuzibandika kwenye mbao za matangazo.

1.3.3.2. Kuendesha uchaguzi wa viongozi wa wanafunzi

Uchaguzi wa kidemokrasia ufanyike kwa kuzingatia kanuni zilizoandaliwa ambapo shughuli zifuatazo zitafanyika:

- Uongozi wa shule kwa kushirikiana na uongozi wa wanafunzi uweke wazi kanuni zote za uchaguzi.
- Uongozi wa shule na walimu uhamasishe wanafunzi kuchukua fomu za kugombea uongozi, kuzijaza na kuzirudisha kwa wakati.
- Majina ya wagombea waliopitishwa yawekwe hadharani.
- Uongozi wa shule utenge siku maalumu kwa ajili ya kampeni na kwa wagombea kujinadi na kuomba kura.
- Mwalimu mwezeshaji kwa kushirikiana na uongozi wa shule kuendesha mafunzo elekezi ya kuwajengea uwezo viongozi waliochaguliwa.

Tafakuri

Mwalimu Mwezeshaji ataongoza tafakuri baada ya kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi wa wanafunzi. Wanafunzi wataandika insha kuhusu uchaguzi na walimu watatoa tathimini yao kuhusu uchaguzi na utendaji wa viongozi wa wanafunzi. Mwalimu Mwezeshaji kwa kushirikiana na walimu wengine watabainisha mambo makuu yaliyojitokeza kwenye maelezo ya wanafunzi na walimu na kisha ataandaa kikao cha walimu na wanafunzi. Maelezo ya walimu na wanafunzi yatahifadhiwa kwenye mkoba wa kazi wa Mwalimu Mwezeshaji. Maswali yafuatayo yatatumika ambapo swali moja au mawili yanaweza kujibiwa katika kikao kimoja:

- Je, tumeweza kufanya uchaguzi wa uongozi wa wanafunzi uliozingatia kanuni za kidemokrasia?
- Je, walimu na wanafunzi wamepokea vipi suala la chaguzi na uongozi wa wanafunzi kuzingatia misingi ya demokrasia?
- Je, ni mabadiliko gani tumeyapata kutokana na kuwajengea wanafunzi uwezo kuhusu uongozi bora unaozingatia misingi ya demokrasia?
- Ni kwa kiwango gani uongozi wa wanafunzi wameweza kuwajibika kwa wanafunzi wenzao?
- Je, ni changamoto zipi zilijitokeza na kutatuliwa na uongozi wa wanafunzi shuleni?

1.4. Kuimarisha shughuli za Ziada za Mtaala katika Kukuza Umahiri wa Demokrasia



Ushiriki wa wanafunzi kwenye shughuli za ziada za mtaala unawezesha kupata matokeo chanya katika kuwawezesha wanafunzi kujifunza na kukuza umahiri wa demokrasia. Katika shughuli hizi wanafunzi wanapewa jukumu kubwa la kuchagua kazi za kufanya na jinsi ya kujifunza. Shughuli hizi zinaweza kugawanywa katika makundi makubwa matatu kama ifuatavyo: kukuza vipaji na ubunifu, taaluma kama vilabu vya masomo na shughuli za kiroho. Unyumbufu uliopo kwenye shughuli za ziada za mtaala unaongeza wigo wa kujifunza kwa wanafunzi.

Malengo:

- Kuwaanda wanafunzi kuthamini na kushiriki katika ulimwengu wa demokrasia.
- Kuimarisha uwezo wa mwanafunzi kushirikiana na kuwa na maadili.
- Kuimarisha uwezo wa wanafunzi kufanya uamuzi wao wenyewe na kuwajibika.
- Kuwaelimisha wanafunzi juu ya umuhimu wa kushiriki katika shughuli za ziada za mtaala.

1.4.1 Kuimarisha umahiri wa demokrasia na uzalendo kwenye klabu za masomo

Klabu za wanafunzi ni moja ya fursa zinazoweza kutumiwa kuimarisha masuala ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji ndani ya shule. Kwa kawaida, klabu hufanyika katika muda wa shughuli za ziada za mtaala ambapo wanafunzi hujiunga katika makundi mbalimbali yenye malengo ya kimasomo au dhima nyinginezo kama jinsia, haki za binadamu, rushwa na mazingira. Kupitia klabu mbalimbali wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza, kujadiliana, kujenga hoja, kuheshimu mawazo ya wengine, kujenga upendo kati yao, uzalendo na kujenga tabia ya kuvumiliana. Tafiti mbalimbali zinaonesha uwepo wa vilabu ingawa katika baadhi ya shule, klabu hizi hazipewi nafasi ya kutosha kuwawezesha washiriki wake kushiriki kikamilifu katika shughuli za klabu. Umahiri huu utawezeshwa kwa kazi zifuatazo.

Kazi Mahususi

1.4.1.1. Walimu na wanafunzi wabainishe fursa mbalimbali za kuboresha ushiriki wa wanafunzi kwenye vilabu:

- Uongozi uandae mkutano wa saa moja kuandaa kanuni za uendeshaji wa vilabu shuleni.
- Uongozi wa shule kuandaa kikao cha walimu na wanafunzi kwa ajili ya kutengeneza kanuni za uchaguzi wa viongozi wa vilabu kuzingatia misingi ya kidemokrasia.
- Uongozi wa shule uandae kikao cha uchaguzi wa viongozi wa vilabu kwa kuzingatia kanuni za kidemokrasia.
- Uongozi wa shule utoe haki sawa katika uchangiaji wa maoni katika kuandaa kanuni kati ya walimu na wanafunzi.

1.4.1.2. Vilabu kujengewa uwezo wa kufanya shughuli zake kwa kufuata misingi ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji.

- Uongozi wa shule uandae warsha ya saa moja kuwajengea uwezo viongozi na washiriki wa vilabu vya wanafunzi juu ya misingi ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji.
- Uongozi wa shule kwa kushirikiana na viongozi wa klabu wapange ratiba ya uendeshaji wa klabu ndani na nje ya shule.
- Uongozi wa shule kwa kushirikiana na viongozi wa vilabu uandae mabango yanayohamasisha kujiunga na vilabu mbalimbali shuleni.
- Uongozi wa shule uweke utaratibu wa kutangaza shughuli za klabu mbalimbali kwa uwazi wakati wa mikusanyiko ya wanafunzi ikiwemo kwenye paredi za asubuhi.
- Uongozi wa shule uweke utaratibu wa kuzingatia jinsia na uwakilishi wa makundi maalumu katika uongozi wa vilabu.

1.4.2. Kuimarisha na kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika michezo kwa kuzingatia mahitaji yao

Michezo na sanaa za utamaduni ni muhimu katika kukuza demokrasia shuleni. Michezo hutoa fursa za ushiriki, ushindani, ujifunzaji, upendo, na kuongeza umahiri katika maeneo mengi kama vigezo muhimu katika kukuza demokrasia. Michezo hutoa fursa za kujifunza maadili yanayosaidia katika kuimarisha demokrasia kwa wanafunzi. Shule nyingi zimekuwa zikitoa nafasi finyu kwa wanafunzi kushiriki katika michezo. Aidha mazoea yamekuwa kuendeleza michezo michache iliyozoeleka kuliko kuja na ubunifu wa kuanzisha michezo mingine itakayoongeza fursa ya watoto wengi kushiriki. Walimu wanapaswa kutambua umuhimu wa michezo, sanaa na utamaduni katika kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji. Michezo inaweza kutumika kama nyenzo ya kusaidia kutatua migogoro, kuhamasisha mijadala, kuvumiliana na kuheshimu tofauti za mawazo.

Kazi Mahususi

1.4.2.1. Ungozi wa shule kushirikiana na wanafunzi kubaini na kuanzisha michezo kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi:

- Kwa kushirikiana na uongozi wa shule andaa kikao cha pamoja na wanafunzi kwa ajili ya kubaini aina ya michezo waipendayo na inayozingatia mahitaji yao. Wanafunzi waongozwe kutambua aina nyingine za michezo zaidi ya mpira wa miguu na mpira wa pete.
- Wakati wa kikao waongoze wanafunzi kuchagua michezo ambayo inaendana na mazingira na uwezo wa shule au jamii husika. Aidha, uchaguzi uzingatie pia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Aidha, katika kikao wahamasishe wanafunzi kujiunga katika fani za kwaya, ushairi, ngoma, na maigizo kama aina nyingine ya sanaa na utamaduni inayoweza kusaidia kuboresha ushiriki wao katika kujifunza kidemokrasia kwa kuwajenga kishindani, kuchaguana katika nafasi za uongozi, kusikilizana, kujenga upendo, na kadhalika.

1.4.2.2. Shule kuweka utaratibu wa kuendesha michezo shuleni kwa kushirikisha wanafunzi:

- Mwalimu Mwezeshaji aandae mafunzo na wanafunzi waweke utaratibu wa uendeshaji wa michezo yote shuleni ikiwemo ratiba.
- Mwalimu Mwezeshaji awaongoze wanafunzi kuchagua viongozi wao wa michezo ngazi ya shule, madarasa au vikosi/mabweni.
- Mwalimu Mwezeshaji ashirikiane na uongozi wa shule na wanafunzi kuandaa viwanja vya michezo na pia katika kununua vifaa vya michezo.

1.4.2.3. Kushirikiana baina ya shule na shule katika michezo:

- Mwalimu Mwezeshaji aandae mafunzo kuhusu umuhimu wa kuwa na mashindano ya shule na shule kama njia ya kuwajenga wanafunzi stadi za kushirikiana.
- Mwalimu Mwezeshaji kupitia mafunzo awaongoze wanafunzi kutambua shule za jirani ambazo wataweza kushirikiana nazo katika michezo, sanaa na utamaduni, na mijadala.
- Mwalimu Mwezeshaji auombe uongozi wa shule kwa niaba ya wanafunzi kuridhia ushirikiano wa shule na shule nyingine kwa kuandika barua kwa shule husika.
- Shule iandae mashindano ya michezo na shule za jirani angalau mara mbili au tatu kwa muhula.
- Shule iandae ratiba ya mashindano ya michezo na shule za jirani ambayo itatambulikwa na kufuatwa.

1.4.3. Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali

Shughuli za uzalishaji mali ni mojawapo ya eneo muhimu linaloweza kusaidia kumjengea mwanafunzi stadi za maisha. Uongozi wa shule umekuwa hautoi fursa kwa wanafunzi kuchagua shughuli za uzalishaji mali na pengine kutofanya kabisa shughuli hizo wakiwa shuleni. Mwanafunzi ataweza kuongeza ujuzi zaidi na kupata fursa ya kufanyia kazi kwa vitendo stadi mbalimbali alizojifunza darasani au nje ya darasa.

Kazi Mahususi

1.4.3.1. Uongozi wa shule kushirikiana na wanafunzi kuainisha shughuli za uzalishaji mali:

- Walimu wawawezeshe wanafunzi kutoa mawazo na kuchagua shughuli ambazo wanaona wataweza kuzitekeleza. Hivyo, wanafunzi waongozwe kuainisha miradi sahihi inayotekelezeka kwenye maeneo yao pamoja na kukubaliana kuhusu matumizi ya bidhaa/ mali zitakazozalishwa.
- Shule iwawezeshe wanafunzi kutenga eneo litakalotumika katika shughuli ya uzalishaji mali na kutambua mahitaji ya kianzio cha uzalishaji.
- Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili mbinu za kupata rasilimali za kuanzisha uzalishaji.
- Walimu wawezeshe wanafunzi kutengeneza uongozi wao ambao utasimamia shughuli za uzalishaji mali ikiwemo uwekaji wa kumbukumbu za mwenendo wa shughuli hizo kama vile gharama zilizotumika, faida zilizopatikana na ufanisi wake wa jumla.
- Shule ihakikishe wanafunzi wote wanajifunza shughuli za uzalishaji mali kwa kupanga ratiba maalumu itakayofuatwa.

1.4.3.2. Uongozi wa shule kwa kushirikiana na wanafunzi waanzishe shughuli za uzalishaji mali:

- Uongozi wa shule usimamie maandalizi ya eneo la uzalishaji mali.
- Walimu wasimamie upatikanaji wa rasilimali za kuanzisha miradi.
- Walimu wasaidie wanafunzi kuanza uzalishaji na kufuatilia utekelezaji wake ili waweze kuboresha shughuli zao za uzalishaji.

1.4.3.3. Kuunda kamati ya usimamizi wa miradi ya shule itakayowahusisha walimu na wanafunzi:

- Shule iwawezeshe wanafunzi kuchagua kamati ya usimamizi wa miradi ya uzalishaji mali shuleni. Wanafunzi wapewe uhuru wa kuchagua walimu ambao wangependa waingie kwenye kamati hii.
- Walimu waliochaguliwa kuingia kwenye Kamati hii wawajengee uwezo wanafunzi walio katika kamati ili wafahamu majukumu yao.
- Kamati ihakikishe inafuatilia utekelezaji wa kazi walizojipangia.
- Shule iandae mkutano mmoja wa kila mwezi wa kutathmini na kupima ufanisi wa maendeleo ya miradi iliyoanzishwa ili kuweza kuboresha uzalishaji.

1.4.3.4. Kamati ya usimamizi wa miradi ya shule kutoa taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu kwenye mbao za matangazo na kwenye mikutano ya shule:

- Kamati iandae ripoti ya utekelezaji ya kila baada ya miezi mitatu ambayo itasomwa kwa wanafunzi wote ili wafahamu mwenendo wa shughuli zao. Ripoti hii ihusishe taarifa za matumizi, mapato, faida au hasara zilizopatikana katika uzalishaji. Hii itasaidia kuongeza uwazi na kujenga motisha kwa wanafunzi waliohusika na uzalishaji.
- Kamati ya usimamizi wa miradi iweke utaratibu wa kuwapongeza waliofanya vizuri katika uzalishaji.

1.4.4. Kukuza na kuendeleza maadili ya kidemokrasia na ari ya uzalendo

Mwanafunzi hawezi kuwa na maadili ya kidemokrasia na ari ya uzalendo bila ya kujifunza. Hivyo shule ni sehemu muhimu katika kuwawezesha wanafunzi kujenga maadili ya kidemokrasia. Mitaala ya elimu imeweka mkazo katika kukuza tabia za kidemokrasia kama vile kuthamini jamii, uwajibikaji, ustahimilivu, uadilifu pamoja na kudumisha amani. Ili wanafunzi waweze kujifunza na kukuwa na tabia hizi lazima wafundishwe kwa vitendo wanapokuwa shule na kwenye jamii. Hata hivyo, shule zimeweka mkazo katika kufundisha maarifa na stadi zaidi kuliko kukuza tabia na mwendo unaokubalika katika jamii. Kutokana na hali hii, jamii inaona kuwa wanafunzi hawajaandaliwa kuishi katika dunia inayobadilika ambayo inasisitiza ustawi wa demokrasia.

Kazi Mahususi

1.4.4.1. Mwalimu wa somo la Uraia kwa kushirikiana na walimu wengine ana jukumu la kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo maadili na tabia za kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji:

- Wanafunzi kuandaa kazimradi kwenye masomo yao zinazolenga kukuza tabia za kidemokrasia kama kulinda mali za Umma, haki za binadamu, upendo, kusaidiana, kuheshimiana, uwajibikaji, uwazi, kutii sheria na taratibu.
- Kutunga na kuimba nyimbo zinazofundisha maadili ya kidemokrasia.
- Wanafunzi kuandika makala za maadili ya kidemokrasia na kuziwazilisha kwenye jumuiya nzima ya shule kupitia mbao za matangazo au hotuba za asubuhi-zilenge yanayotokea shuleni na kwenye jamii.
- Kushiriki kwenye kazi za kijamii zenye kuonesha matendo ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji.
- Shule kuwatambua wanafunzi vinara wa kukuza maadili ya kidemokrasia na uzalendo na kuwapa nafasi ya kutoa elimu.
- Kuendesha midahalo ya wanafunzi inayolenga maadili ya kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji ndani na nje ya shule.
- Shule iwape motisha vinara wa kuongoza maadili ya kidemokrasia na uzalendo.

Tafakuri



Mwalimu Mwezeshaji kwa kushikirikina na walimu wengine wataanda vikao vya kufanya tafakuri ambayo wanafunzi watapewa nafasi kubwa ya kutoa maoni yao. Vikao hivi vitafanyika baada ya ratiba rasmi ya masomo ya darasani. Kila kikao kitalenga eneo mahususi kama vile ushiriki katika klabu, michezo na shughuli za uzalishaji mali na maadili ya demokrasia. Wanafunzi watatoa maelezo kwa maandishi na walimu watayachambua kwa kushirikiana na uongozi wa wanafunzi ili kubaini hoja kuu zitakazojadiliwa kwenye vikao. Maswali yafutayo yatatumika:

- Wanafunzi wameitikiaje uhamasishaji wa masuala ya klabu shuleni unavyohusishwa na umahiri wa demokrasia na uzalendo?
- Je, klabu zinaendeshwa kidemokrasia?
- Kwa kiwango gani klabu zinatumika kukuza umahiri wa kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji kwa wanafunzi?
- Kwa kiwango gani ushiriki katika michezo ni jumuishi?
- Ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za uzalishaji mali ukoje?
- Wanafunzi wamewezeshwa kubuni na kufanya kazimradi zinazolenga kukuza mwenendo wa kidemokrasia, uzalendo na uwajibikaji?





Moduli 2:

Mbinu na Mikakati ya Kukuza Demokrasia, Uzalendo na Uwajibikaji wa Wanafunzi kwenye Jamii

Familia na jamii ni nguzo muhimu katika kuwalea na kuwajengea wanafunzi umahiri wa demokrasia, uzalendo na uwajibikaji. Katika ngazi ya familia wazazi wana nafasi ya kuwapa watoto wao nafasi ya kushiriki na kuchangia katika maisha ya kila siku ya familia kwa kutoa mawazo na kutekeleza majukumu mbalimbali. Katika ngazi ya jamii, wanafunzi wanawezeshwa kutumia fursa zilipo kuchangia katika maendeleo ya jamii kwa kuyaweka katika vitendo wanayojifunza shuleni.

Malengo ya moduli hii ni:

01 Kuimarisha fursa za wanafunzi kushiriki katika michakato ya demokrasia katika jamii.

02 Kuwawezesha wanafunzi kutumia umahiri wa demokrasia na ari ya uzalendo katika jamii.

03 Kuwawezesha wanafunzi na kutumia majukwaa mbalimbali kubaini fursa na changamoto zilizopo na jinsi ya kuzitatua.

04 Kuwawezesha wanafunzi kupaza sauti kuhusu masuala yanayohusu ushiriki wao katika shughuli za kijamii.

05 Kuwawezesha wanafunzi kujenga ushirikiano mzuri na jamii yao.

Kazi Kuu:

2.1. Kuandaa Utayari wa Jamii

Ili elimu itolewayo shuleni hususani demokrasia na uzalendo kwa wanafunzi iweze kuwa na matokeo chanya, shule inapaswa ifungue milango ya kimawasiliano kati ya familia na wanajamii wengine. Wanafunzi hujifunza vizuri zaidi pale wazazi wao na wanafamilia wanapopenda kujihusisha na shule na masuala ya elimu kwa ujumla. Tunapozihusisha familia katika kujifunza kwa mwanafunzi, kunaongeza wigo wa kuhusisha wanayojifunza shuleni na maisha ya kila siku. Ushirikiano wa familia, wanajamii na shule una umuhimu mkubwa katika kujenga demokrasia, uzalendo na uwajibikaji wa kweli kwa wanafunzi. Kutokana na uhalisia huu na umuhimu ni vyema kuelimisha jamii yetu umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Kazi Mahususi

2.1.1. Mwezeshaji Jamii kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji/mtaa/ dini/ kuandaa mkutano wa siku moja usiozidi saa mbili kwa viongozi wa mtaa/ kijiji kuhusu dhana ya demokrasia, uzalendo na uwajibikaji. Mkutano utakuwa na agenda zifuatazo:

- Kujadili umuhimu wa uwepo wa demokrasia ya wanafunzi katika jamii.
- Kujadili umuhimu wa ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za kijamii zinazolenga kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji.
- Kujadili changamoto za ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za jamii.
- Kujadili namna ya kuzitatua changamoto za ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za kijamii.
- Kujadili namna ya kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli za kijamii.

2.1.2. Mwezeshaji Jamii ataandaa mkutano kwa kushirikiana na uongozi wa kata usiozidi saa moja kujadili namna ya kuwashirikisha wanafunzi katika masuala ya kijamii yanayolenga kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji. Mkutano utakuwa na agenda zifuatazo:

- Kuhamasisha na kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli mbalimbali za kijamii zinazolenga kukuza demokrasia.

- Kubaini changamoto za ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za jamii
- Kujadili namna ya kuzitatua changamoto zilizobainishwa za ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za jamii.

2.1.3. Mwezeshaji Jamii kuandaa vipeperushi mbalimbali vya kuelimisha wanafunzi na jamii kuhusu umuhimu wa demokrasia:

- Kuwasiliana na Mwezeshaji wa mradi pamoja na uongozi wa kata jinsi ya kupata rasilimali fedha za kutengenezea vipeperushi hivyo.
- Mwezeshaji Jamii pamoja na uongozi wa kata kuandaa utaratibu wa namna ya kuvigawa vipeperushi vilivyotengenezwa/vitakavyoandaliwa.
- Kushirikiana na Baraza la Wanafunzi na Watoto katika kutoa elimu kwa vijana.
- Kutumia sanaa za maonesho kutoa elimu ya demokrasia na uzalendo.
- Kuandaa na kuendesha makongamano ya kukuza hamasa kwa wanafunzi kushiriki katika demokrasia.
- Kuandaa makongamano mbalimbali kwa ajili ya kujadiliana na kuamsha ari ya kushiriki shughuli za kidemokrasia na kuwa wazalendo.



Tafakuri

Mwezeshaji Jamii kwa kushirikiana na Mwalimu Mwezeshaji wataanda au kutumia vikao rasmi vya kijamii (kama vile mkutano mkuu wa kijiji) kuchambua jinsi jamii inavyotekeleza jukumu lake la kuwajengea wanafunzi umahiri wa demokrasia. Maelezo ya wanajamii yatahifadhiwa kwenye mkoba wa kazi wa Mwalimu Mwezeshaji na Mwezeshaji Jamii . Maswali yafuatayo yatatumika wakati wa tafakuri:

- Je, mwitikio wa wanajamii kuhusu ushiriki wa wanafunzi kwenye masuala ya kijamii ukoje?
- Je, kuna miongozo ya kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika shughuli za kijamii?
- Majukumu ya wanafunzi katika kujenga jamii ya kidemokrasia yamebainishwa na fursa zilizopo?
- Vijana ambao sio wanafunzi wamepokeaje wazo la wanafunzi kushiriki katika shughuli za kijamii?

Kazi Kuu:

2.2. Kuimarisha Ushiriki wa Wanafunzi kwenye Shughuli za Kijamii

Katika kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji wa wanafunzi kwenye jamii, jukumu kubwa litakuwa kuandaa mazingira wezeshi ambayo wanafunzi wote wataweza kushiriki na kujumuishwa katika kupanga na kutoa uamuzi ya masuala yote yanayohusu jamii husika. Mazingira wezeshi yatasaidia wazazi na wanajamii kuunga mkono programu ya kukuza demokrasia kwa wanafunzi ndani ya jamii. Hali ilivyo katika jamii zetu, wanafunzi wamekuwa hawashiriki na hakuna juhudi za makusudi na za kutosha za kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za jamii. Ikumbukwe kuwa bila kujenga mazingira wezeshi katika jamii kuhusu demokrasia na uzalendo kwa wanafunzi kunawakosesha fursa, umahiri na utashi wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii. Kazi zifuatazo ni muhimu:

Kazi Mahususi

2.2.1. Kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika shughuli za kijamii na kutoa maoni yao:

- Kuandaa na kuhamasisha wanafunzi ili kushiriki katika mikutano ya kijiji/ Mtaa/ Kata na kuchangia hoja.
- Kutoa maelezo ya kina kwa wanafunzi kuhusu ushiriki wao katika mikutano husika.
- Kuhusisha wanafunzi katika kutoa matangazo.
- Kutoa nafasi kwa wanafunzi kuhoji mambo ya msingi na kupatiwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali yanayohusiana na demokrasia.
- Kuwapa wanafunzi nafasi za uongozi katika shughuli za kijamii.

2.2.2. Kuanzisha vikundi vya wanafunzi ambavyo vitashirikiana na jamii na makundi mengine kutekeleza shughuli za kijamii:

- Kuandaa wanafunzi (mwalimu na mwezeshaji jamii) kwa kuwapa maelezo kuhusu kazi wanayoenda kufanya kwa kushirikiana na jamii.
- Kutoa maelekezo yanayojitosheleza ya jinsi watakavyoshirikiana na wanajamii katika kutekeleza kazi husika.
- Kuwapatia fursa wanafunzi kuhoji ushirikishwaji wao na jamii katika shughuli mbalimbali za kijamii.
- Wazazi na wadau wengine kualikwa shuleni mara kwa mara katika kufanya uamuzi kuhusu maendeleo ya shule.

2.2.3. Kuanzisha mifumo ya kupokea na kusikiliza sauti za wanafunzi. Ili kufanikisha hili mwalimu na mwezeshaji jamii wafanye yafuatayo:

- Mwalimu na Mwezeshaji jamii kuwasiliana na uongozi wa Kata ili kuandaa mkutano kati ya Diwani na wanafunzi ili wanafunzi waweze kupata maelezo ya jinsi wanavyoweza kushiriki na kuwasilisha hoja zao katika mikutano ya Kata.
- Katika kikao cha diwani na wanafunzi, diwani ataombwa awape fursa wanafunzi kushiriki katika kikao cha madiwani kama wageni wake ili wakajifunze namna demokrasia inafanya kazi ngazi ya vikao vya madiwani.
- Kuwepo na siku maalumu ya kuwasikiliza vijana/wanafunzi.
- Jamii kutoa fursa kwa wanafunzi kushiriki katika shughuli/kazi za kijamii.
- Kuandaa mkutano na viongozi wa kijiji/mtaa/kata kueleza dhima ya ushiriki wa wanafunzi kwenye masuala ya demokrasia.
- Kuwepo na masanduku ya maoni ngazi ya kata/Kijiji/mtaa na majibu yatolewe katika mbao za matangazo za kijiji/mtaa/kata.

Tafakuri

Ili kuhakikisha yaliyopangwa yanafanyika kuhusiana na ushiriki wa wanafunzi katika suala la kukuza demokrasia ni muhimu kufanya tafakuri ya utekelezaji wake. Mwezeshaji Jamii akishirikiana na Mwalimu Mwezeshaji waandae vikao kila mwezi kati ya wanafunzi na viongozi wa vijiji kutafakuri kuhusu ushiriki wa wanafunzi katika masuala ya kijamii. Taarifa za tafakuri zihifadhiwe kwenye mkoba wa kazi wa mwezeshaji jamii na mwalimu: Pia tafakuri ziwekwe katika mbao za matangazo ngazi ya Kijiji/Mtaa/Kata ili ambaye hakuwepo katika kikao apate taarifa. Maswali haya yatumike katika tafakuri:

- Ni hatua gani zichukuliwe katika kutatua changamoto hizo?
- Je, wanafunzi wamelipokeaje suala la kushiriki katika shughuli za kijamii?
- Je, uhusiano kati ya wanafunzi na jamii ukoje?
- Je, wanafunzi wameweza kujifunza nini katika ushiriki wao kwenye shughuli ya kijamii?
- Uongozi wa Kijiji umelipokeaje suala la kushirikisha wanafunzi katika shughuli tofauti za kijamii?
- Ni changamoto gani zimejitokeza katika ushiriki wa wanafunzi kwenye shughuli za kukuza demokrasia?

Kiambatisho: mwongozo wa tathmini.

Inatarajiwa kwamba kama mdau muhimu wa kutekeleza kivunge hiki utawajibika kuhakikisha malengo ya kivunge hiki yanafikiwa kama yalivyopangwa na muongozo ufuatao utakusaidia kutathimini utekelezaji wa kazi za kutendwa na kazi mahususi kama zilivyoainishwa kwenye jedwali namba 1.

Viashiria vya utendaji na vigezo vya tathmini

Kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji wa wanafunzi Shuleni.

Kazi za kutendwa	Kiashiria cha utendaji	Kiwango cha utendaji			
		Dhaifu	Wastani	Nzuri	Nzuri sana na Endelevu
1.1.1 Kuimarisha uelewa walimu kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia.	Misingi ya demokrasia inaakisiwa katika ujifunzaji na ufundishaji.	Ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia unatajwa ila haujitokezi popote.	Maandalizi ya walimu yanabeba dhana ya ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia.	Ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia umejitokeza kwenye maandalizi ya walimu na unatekelezwa darasani.	Ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia unasisitizwa kwenye miongozo ya shule na unatekelezwa darasani kwa ufanisi mkubwa.
1.1.2 Kuimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia.	Ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia unafahamika vema na kuzingatiwa na wanafunzi.	Ujifunzaji na ufundishaji wa kidemokrasia unatajwa na wanafunzi ila hawauzingatii katika kujifunza.	Wanafunzi wamebeba dhana ya ujifunzaji na ufundishaji kidemokrasia ila hawaizingati sana mwalimu anapoitumia.	Wanafunzi wanapenda kujifunza kwa mbinu za kidemokrasia na wanafurahia somo mwalimu anapozitumia.	Wanafunzi na wanashiriki kwa ufanisi mkubwa kwenye kujifunza mwalimu anapotumia mbinu za kidemokrasia na wanafanya hivyo hata nje ya darasa.

1.2.1 Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kushirikisha wanafunzi kwenye uamuzi.	Uongozi wa shule unawashirikisha wanafunzi kwenye uamuzi wote unaohusiana na wanafunzi na shule.	Ushirikishwaji wa wanafunzi kwenye uamuzi unatajwa shuleni ila hautekelezwi.	Uongozi wa shule umebeba dhana ya ushirikishwaji wa wanafunzi kwenye uamuzi na wanawashirikisha baadhi ya uamuzi.	Wanafunzi wanashirikishwa kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi.	Ushirikishwaji wa wanafunzi kwenye uamuzi umewekwa kwenye miongozo na unatekelezwa shuleni kwa kiwango kikubwa.
1.2.2 Kuimarisha mfumo wa wanafunzi kupaza sauti.	Shule ina mifumo ya kuwawezsha wanafunzi kutoa maoni yao na kujieleza kwa uhuru.	Mifumo ya kupaza sauti ipo ila haitumiki kama inavyotakiwa.	Mifumo ya kupaza sauti ipo ila wanafunzi wachache sana wanaitumia kutoa maoni au mitazamo yao kuhusu mambo mbalimbali.	Mifumo ya kupaza sauti ipo na shule inasisitiza wanafunzi kuitumia kutoa maoni yao. Wanafunzi wengi wanafanya hivyo.	Mifumo ipo na shule inasisitiza wanafunzi kuitumia kutoa maoni yao. Wanafunzi wengi wanafanya hivyo na uongozi wa shule unatoa mrejesho.
1.3.1 Kuimarisha utayari wa uongozi wa shule kuthamini demokrasia katika uongozi wa wanafunzi.	Uongozi wa wanafunzi unasikilizwa na kuwezesha katika kutekeleza majukumu yao.	Uongozi wa wanafunzi unasikilizwa kidogo na haupewi nyezo na uwezo wa kutekekeza majukumu yake.	Baadhi ya walimu wanajali na kutoa ushirikiano kwa uongozi wa wanafunzi. Ila kwa sehemu kubwa unatekeleza uamuzi ya uongozi wa shule.	Uongozi wa wanafunzi unapatiwa mafunzo ya uongozi na kupewa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa walimu wengi na uongozi wa shule.	Uongozi wa wanafunzi unapatiwa mafunzo ya uongozi na kupewa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa walimu wote na uongozi wa shule. Pia viongozi wanapatiwa nyezo za utendaji.
1.3.2 Kuimarisha uchaguzi viongozi wa wanafunzi.	Uongozi wa wanafunzi unapatikana kidemokrasia.	Uongozi wa wanafunzi unapatikana kwa njia ya uteuzi na kujitolea.	Baadhi ya uongozi wa wanafunzi unapatikana kwa uchaguzi usiozingatia misingi ya kidemokrasia.	Baadhi ya kanuni za kuchagua viongozi wa shule zimeandikwa na kubandikwa kwenye mbao za matangazo na viongozi wote wanapatikana kidemokrasia.	Kanuni za kuchagua viongozi wa shule zimeandikwa na kubandikwa kwenye mbao za matangazo na viongozi wote wanapatikana kidemokrasia.

1.4.1 Kuimarisha umahiri wa demokrasia na uzalendo kupitia klabu za masomo.	Wanafunzi wote shuleni wanashiriki kwenye klabu za masomo.	Wanafunzi wengi hawashiriki kwenye klabu za masomo.	Wanafunzi wachache wanashiriki kwenye klabu za masomo.	Shule ina klabu za aina mbalimbali na wanafunzi wote wanashiriki kwenye klabu za masomo.	Shule ina klabu za aina mbalimbali na wanafunzi wote wanashiriki na kuna ubunifu wa aina mbalibali kwenye klabu.
1.4.2 Kuimarisha na kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi kwenye michezo kwa kuzingatia matakwa yao.	Wanafunzi wote wanashiriki kwenye michezo kwa mujibu wa matakwa yao.	Wanafunzi wengi hawashiriki kwenye michezo na shule ina michezo michache.	Wanafunzi wachache wanapata nafasi ya kushiriki kwenye michezo.	Wanafunzi wengi wanashiriki kwenye michezo wanayoipenda ila shule haina vifaa vya kutosha.	Wanafuzi wengi wanashiriki kwenye michezo wanayoipenda ikiwemo michezo ya asili. Shule ina vifaa vya kutosha.
1.4.3 Kuimarisha shughuli za Uzalishaji Mali.	Shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinaendeshwa shuleni na wanafunzi wanashiriki kwa mwitikio mkubwa.	Hakuna shughuli za uzalishaji mali shuleni.	Shughuli chache za uzalishaji mali zinafanyika shuleni na wanafunzi wachache wanashiriki.	Shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinafanyika kwa uwazi shuleni na wanafunzi wengi wanashiriki.	Shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinafanyika kwa uwazi shuleni na wanafunzi wengi wanashiriki wanaonesha ubunifu.
1.4.4 Kukuza na kuendeleza maadili ya kidemokrasia na ari ya uzalendo.	Wanafunzi wanazingatia maadili ya kidemokrasia na misingi ya uzalendo.	Wanafunzi hawafahamu maadili ya Kidemokrasia na uzalendo.	Wanafunzi wachache wanafahamu maadili ya kidemokrasia na matendo ya kizalendo lakini hawatekelezi kwa vitendo.	Wanafunzi wanafamu maadili ya kidemokrasia na uzalendo na wanayatekeleza kwa vitendo.	Wanafunzi wengi wanafamu maadili ya kidemokrasia na uzalendo, wanayaishi kwa vitendo katika mazingira ya shule na kwenye jamii.

Kukuza demokrasia, uzalendo na uwajibikaji wa wanafunzi kwenye Jamii.					
2.1 Kuimarisha Utayari wa Jamii.	Wanafunzi wanashiriki katika fursa mbalimbali za kidemokrasia na wana matendo ya kizalendo.	Jamii imebeba dhana ya demokrasia ila haitoi nafasi kwa wanafunzi kuchangia au kujihusisha na maswala ya kidemokrasia na uzalendo.	Jamii inatoa nafasi kwa wanafunzi wachache kushiriki shughuli mbalimbali ya kidemokrasia na uzalendo.	Jamii inatoa nafasi kwa wanafunzi wengi kushiriki katika shughuli mbalimbali ya kidemokrasia na uzalendo lakini wanafunzi hawahamasishwi.	Dhana ya ushiriki wa wanafunzi katika michakato ya kidemokrasia na uzalendo imebebwa na jamii na mikakati ya kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi imewekwa bayana na inatekelezwa.
2.2 Kuimarisha ushiriki wa wanafunzi kwenye shughuli za kijamiii.	Wanafunzi wanashiriki shughuli mbalimbali za kijamii.	Wanafunzi hawashiriki shughuli za kijamii.	wanafunzi wachache wanashiriki shughuli za kijamii pale wanapoambiwa.	wanafunzi wengi wanashiriki shughuli za kijamii kwa kujitolea.	wanafunzi wengi wanashiriki shughuli za kijamii kwa jujitolea na taratibu za kuhakikisha wanafunzi wanashiriki zimewekwa bayana.

HakiElimu ni asasi ya kiraia inayowawezesha wananchi kufanya mabadiliko katika elimu na demokrasia

S.L.P 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (0)22 2151852/3
Fax:+255 (0)22 2152449
Barua Pepe: info@hakielimu.or.tz
Tovuti: www.hakielimu.or.tz

@hakielimu